# UFUNUO 2



COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.




[1] MUHURI WA TANO WAELEZA NGUVU ZA MAOMBI WANAPOMUOMBA MUNGU ALIPE KISASI.


ALLAH AKBAR! MUNGU TU NDIYE MKUU. HAKUNA WAKRISTO WATAKAOKUBALIWA KUISHI KATIKA MJI HUU.
MPAKA LINI MUNGU HURU, MTAKATIFU NA WA KWELI, HADI UHUKUMU WAKAAZI WA ULIMWENGU NA KULIPIZA DAMU YETU? [1]
LAZIMA UNGOJE MDA MREFU ZAIDI MPAKA IDADI YA NDUGU ZAKO WANAOFAA KUULIWA IKAMILIKE.
UFUNUO 6:9-11




[1] MIGAWANYIKO YA ARDHI INAANZA KUVUNJIKA KWA WAKATI MMOJA, HUKU IKISABABISHA ARDHI KUWA NA MITETEMEKO YA ARDHI AMBAYO HAIJAWAHI KUONEKANA MBELENI.

[2] INAWEZEKANA NI KWA SABABU YA KIASI KIKUBWA CHA JIVU NA UCHAFU UNAOPULIZWA ANGANI KUTOKA MILIPUKO YA VOLKENO IKIFUATANA NA MTETEMEKO WA ARDHI. HII PIA ILITABIRIWA KATIKA AGANO LA KALE (YOELI 2:31).

[3] KUNA UWEZEKANO MKUBWA HII NI LIMONDO KUBWA AU MVUA YA KIMONDO INAYOPIGA ARDHI.

[4] WENYEJI ULIMWENGUNI WATAANZA KUGUNDUA CHANZO CHA MATUKIO HAYA.

[5] MUHURI WA SITA UNAANZA WAKATI NABII ANAUITA "SIKU YA BWANA." MIHURI TANO YA KWANZA NI MATOKEO YA SHUGHULI ZA BINADAMU, LAKINI SASA MUNGU ANAANZA KUINGILIA KATI MOJA KWA MOJA.


"JUA LIKAWA GIZA KAMA GUNIA LA NYWELE ZA MBUZI, MWEZI WOTE UKAGEUKA KAMA DAMU, [2] NA NYOTA ZIKAANGUKA JUU YA NCHI, [3] KAMA VILE MTINI UPUKUTISHAVYO MAPOOZA YAKE UTIKISWAPO NA UPEPO MWINGI."
"MBINGU ZIKAONDOLEWA KAMA UKURASA ULIVYOKUNJWA, NA KILA MLIMA NA KISIWA KIKAHAMISHWA KUTOKA MAHALI PAKE."
"WOTE DUNIANI - WAFALME, WANA WA WAFALME, MAJEMEDARI, NA MATAJIRI, NA WENYE NGUVU, NA KILA MTUMWA NA KILA MWUNGWANA WALIJIFICHA KATIKA PANGO NA CHINI YA MIAMBA YA MILIMA."
UFUNUO 6:12-1


"NIKAONA MALAIKA WANNE WAMESIMAMA KATIKA PEMBE NNE ZA DUNIA. WALIZIZUIA PEPO NNE ZA NCHI UPEPO USIVUME JUU YA NCHI WALA JUU YA BAHARI."
"NIKAMUONA MALAIKA MWENGINE AKIPANDA KUTOKA MAAWIO YA JUA, MWENYE MUHURI WA MUNGU ALIYE HAI."
MSIIDHURU NCHI, WALA BAHARI, WALA MITI HADI TUTAKAPOWATIA MUHURI WATUMWA WA MUNGU KWENYE VIPAJI VYA NYUSO ZAO.
"KATIKA KILA YA KABILA KUMI NA MBILI MUNGU ALIWAPIGA MUHURI NA KUWACHAGUA ELFU KUMI NA MBILI WA KUMTUMIKIA WAKATI HUU."[1]
[1] HAWA NI WAYAHUDI WA KWANZA WALIOKOMBOLEWA HATIMAYE ISRAELI INAPOANZA KUWA NCHI YA USHUHUDA AMBAYO MUNGU ALIITA KUWA KATIKA AGANO LA KALE.
HAWA WAINJILISTI WA KIYAHUDI 144,000 WALIKUWA WASHIRIKI WAKUU WAMISHONARI AMBAO MUNGU ALIWALINDA HUKU AKIWATUMIA KUTANGAZA INJILI KOTE DUNIANI KWA WAYAHUDI NA WAYUNANI.



UFUNUO 7:1-8




"BAADA YA HAYO NILITAZAMA NIKAONA MKUTANO MKUBWA SANA AMBAO HAPANA MTU AWEZAYE KUHESABU."
"WATU WA KILA TAIFA NA KABILA, NA JAMAA, NA LUGHA NCHINI. [1] WAMESIMAMA MBELE YA KITI CHA ENZI - NA MBELE YA MWANA-KONDOO."
WOKOVU UNA MUNGU WETU AKETIYE KATIKA KITI CHA ENZI, NA MWANA-KONDOO.
[1] INGAWA WAKATI HUU UTAKUWA WAKATI WA HUKUMU ISIYO NA KIFANI, PIA UTAKUWA WAKATI WA WOKOVU USIO NA KIFANI, NA WENGI WAKIWA NA IMANI WAKATI HUU WA DHIKI.
UFUNUO 7:9-10



AMINA!


AMINA!
BARAKA NA UTUKUFU NA HEKIMA NA SHUKRANI NA HESHIMA NA UWEZA NA NGUVU ZINA MUNGU WETU HATA MILELE NA MILELE.
UFUNUO 7:11-12


NANI HAWA, WALIOVIKWA MAVAZI MEUPE, NA WAMETOKA WAPI?
BWANA, WAJUA.
HAO NDIO WANATOKA KATIKA DHIKI KUU. [1] WAMEFUA MAVAZI YAO NA KUYAFANYA MEUPE KATIKA DAMU YA MWANA-KONDOO. [2]
KWA HIYO WANAMTUMIKIA MCHANA NA USIKU...YEYE AKETIYE KWENYE KITI CHA ENZI ATATANDA HEMA LAKE LA UWEPO WAKE JUU YAO.
"HAWATAONA NJAA TENA...WALA HAWATAONA KIU TANA...WALA JUA HALITAWAPIGA WALA HARI ILIYO YOTE."
"NA MUNGU ATAFUTA MACHOZI KUTOKA MACHO YAO."
[1] KATIKA MIAKA SABA YA WAKATI WA DHIKI WENGI WATAOKOKA, KUSHAHIDI NA KUINGIA MBINGUNI.
[2] MAVAZI YAO NI MEUPE - KRISTO AMEWATAKASA KUTOKA DHAMBI ZAO.


"ALIPOIFUNGUA MUHURI YA SABA, KUKAWA KIMYA MBINGUNI KAMA MUDA WA NUSU SAA." [1]
"NIKAWAONA MALAIKA SABA WASIMAMAO MBELE YA MUNGU NAO WAKAPEWA BARAGUMU SABA."
"MALAIKA ALIPEWA UBANI MWINGI WA KUTOA PAMOJA NA MAOMBI YA WATU WA MUNGU YALIYOENDA JUU MBELE YA MUNGU."
"BAADA YA HIVI MALAIKA HUYO ALICHUKUA MOTO KUTOKA KWA MADHABABU NA KUURUSHA ARDHINI - NA KUKATOKEA NGURUMO, KUGURUMA, MWANGA WA UMEME NA MTETEMEKO WA ARDHI."
"NA WALE MALAIKA SABA WENYE BARAGUMU SABA WAKAJIFANYA TAYARI ILI WAZIPIGE."
[1] KIMYA HIKI KINASABABISHWA NA KUSTAAJABU NA MATARAJIO YANAYOTOKANA NA UKWELI WA KUTISHA WA HUKUMU AMBAZO MUNGU YUKO KARIBU KUITOLEA ARDHI.

UFUNUO 8:1-6


"MALAIKA WA KWANZA ALIPOPIGA BARAGUMU, KUKAWA MVUA YA MAWE NA MOTO VILIVYOTANGAMANA NA DAMU, VIKATUPWA JUU YA NCHI."
[1] HII YAWEZA KUWA MILIPUKO YA VOLKENO KUTOKANA NA MITETEMEKO YA ARDHI. MVUKE NA MAJI YANAYOTOLEWA NA MILIPUKO HII YAWEZA KUFANYA MATONE YA MVUA YA MAWE PAMOJA NA LAVA YA MOTO. KIOEVU NA GESI YA SUMU INAYOFUATIA YAWEZA KUWA NYEKUNDU KAMA DAMU.



"MOTO ULIKUWA MKUU MNI HATA THELUTHI YA NCHI IKATEKETEA KWENYE MOTO." [1]
"THELUTHI YA MITI NA THELUTHI YA NYASI KWENYE NCHI ZIKATEKETEA."





[1] HII YAWEZA KUWA KIMONDO KUBWA INAYOWAKA INAPOINGIA ANGA YA ARDHINI.

[2] HII YAWEZA KUWA IMETOKANA NA KIMONDO, AMA KUTOKA MAWIMBI MEKUNDU AMBAPO VIDUDU VILIVYOKUFA VINAFANYA SUMU MAJI - AU HATA YAWEZA KUWA DAMU - TENDO LA WAZI KABISA LA HUKUMU YA KIUNGU.

[3] KUNA UWEZEKANO MKUBWA KIMONDO KIKUBWA KINATENGENEZA WIMBI KUBWA VILE VILE LINALOANGAMIZA THELUTHI YA MERIKEBU ZA DUNIA.


"THELUTHI YA BAHARI IKAWA DAMU, WAKAFA THELUTHI YA VIUMBE VILIVYOMO KATIKA BAHARI VILIVYO NA UHAI [2] THELUTHI YA MERIKEBU ZIKAHARIBIWA." [3]
UFUNUO 8:8-9


MALAIKA WA TATU AKAPIGA BARAGUMU, NYOTA KUBWA, ILIYOKUWA IKIWAKA KAMA TAA IKAANGUKA KUTOKA MBINGUNI. [1] IKAANGUKA KWENYE THELUTHI YA MITO NA JUU YA CHEMCHEMI ZA MAJI."
"NA JINA LAKE ILE NYOTA YAITWA PAKANGA; THELUTHI YA MAJI YAKAWA UCHUNGU - NA WANADAMU WENGI WAKAFA KWA MAJI HAYO YALIYOGEUKA UCHUNGU."
[1] MWILI MWINGINE WA MBINGUNI ULISAMBARATIKA JUU YA ARDHI NA KUSABABISHA MAJI KUWA UCHUNGU. KUTOKA MAELEZO "KUWAKA KAMA TAA", YAWEZA KUWA KIMONDO INAYOPIGA ARDHI.



UFUNUO 8:10-11




[1] WANATHEOLOJIA WENGI WANAAMINI THELUTHI YA MIILI YA MBINGUNI KUWA GIZA NI KUONYESHA THELUTHI YA MAPEPO WALIOANGUKA NA IBILISI KUTOKA MBINGUNI.


"THELUTHI YA MCHANA ISIANGAZE WALA USIKU VIVYO HIVYO." [1]
OLE OLE OLE WAO WAKAAO JUU YA NCHI! KWA SABABU YA SAUTI ZISALIAZO ZA BARAGUMU NA MALAIKA WATATU WALIO TAYARI KUPIGA!
UFUNUO 8:12-13




[1] KAWAIDA MAISHA YA NZIGE NI KAMA MIEZI MITANO NA NZIGE HAWA WA KIPEPO WANA MUDA WA MAISHA UNAOKARIBIA HUO.

[2] KUTAFUTA KUMALIZA KUTESEKA KATIKA KIFO, WATU WATAPATA MAJARIBIO YA KUJIUA YATAAMBULIA PATUPU.


MSIZIDHURU NYASI WALA MIMEA AU MITI. WADHURU TU WASIO NA MUHURI YA MUNGU KWENYE VIPAJI VYA NYUSO ZAO.
MSIWAUE - MWAWEZA KUWATESA TU KWA KIPINDI CHA MIEZI MITANO. [1]
MTU ANIOKOE - UCHUNGU HUU NI MKALI!
NIACHE NIFE - NIACHE NIFE!




[1] KAMA VILE KUNA UONGOZI WA MALAIKA KUNA UONGOZI WA MAPEPO. MALAIKA HUYU WA SHIMO LISILOKUWA NA MWISHO NI MMOJA WA VIONGOZI WAKUU WA IBILISI, LABDA HATA IBILISI MWENYEWE.



"OLE WA KWANZA UMEKWISHA... TAZAMA BADO ZIKO OLE MBILI ZINAKUJA BAADAYE."
UFUNUO 9:7-


[1] MTO MKUBWA FRATI ULIKUWA MOJAWAPO WA MITO MINNE ILIYOPITA KATIKATI YA SHAMBA LA EDENI. KUANZIA BABELI ENEO HILI LILIZAA DINI NYINGI ZA KIPAGANI DUNIANI.
[KUMBUKA] KAWAIDA MADHABAHU NI MAHALI AMBAPO MUNGU ALIJIBU MAOMBI YA WATU WAKE YA REHEMA - LAKINI SASA MADHABABHU ITAJIBU NA KILIO CHA KULIPIZA KISASI.


"MALAIKA WANNE WALIOKUWA WAMETAYARISHWA KWA SAA, SIKU, MWEZI, NA MWAKA, WALIACHILIWA KUWAUWA THELUTHI YA BINAADAMU."
WAFUNGUE MALAIKA WANNE WALIOFUNGWA KWENYE MTO MKUBWA FRATI. [1]


"NILISIKIA IDADI YA MAJESHI WAPANDA FARASI; ILIKUWA MILIONI MIA MBILI." [1]
MAMA YANGU ALIJARIBU KUNIFANYA NIISOME BIBILIA - KUSEMA KUWA HAYA YANGETENDE-KA. MBONA SIKUMSIKIZA! NI ZAIDI YA VILE NILIWAHI KUDHANI.
MUNGU NIREHEMU - MIMI MWENYE DHAMBI.
THELUTHI YA BINAADAMU WALIULIWA NA TAUNI TATU ZA MOTO, MOSHI NA SALFA ILIYOTOKA MIDOMONI MWAO.
[1] JESHI LA KIPEPO LINAACHILIWA NA KUUWA THELUTHI YA BINAADAMU WALIOBAKI.


"AMBAO HAWAKUULIWA NA TAUNI HIZI BADO HAWAKUTUBU KWA KAZI YA MIKONO YAO."
"WALIENDELEA KUABUDU MAPEPO NA MIUNGU YA DHAHABU, FEDHA, SHABA, JIWE NA MBAO - MIUNGU ISIYOONA WALA KUSIKIA AU KUTEMBEA."
"HAWAKUTUBU KWA AJILI YA MAUAJI YAO, UCHAWI WAO,,,"
"...KUZINI KWA AU WIZI WAO."
XXX
GIRLS
GIRLS
GIRLS
GIRLS
LIVE
XXX
UFUNUO 9:16



"KISHA MALAIKA MWENGINE MWENYE NGUVU ALISHUKA KUTOKA MBINGUNI."
YATIE MUHURI MANENO YALIYONENWA NA NGURUMO SABA NA WALA USIYAANDIKE.
KWA JINA LA MUNGU PEKEE WA KWELI NA AISHIYE KUTAKUWA HAKUNA TENA KUKAWIA!
"LAKINI WAKATI HUU MALAIKA WA SABA AKIWA TAYARI KUPIGA BARAGUMU HAPO NDIO SIRI YA MUNGU ITATIMIZWA [1] - KAMA ALIVYOWAHUBIRI MANABII WAKE."
[1] KATIKA AGANO JIPYA SIRI NI UKWELI ULIOFICHWA LAKINI UMEFUNULIWA KUPITIA KRISTO NA MITUME WAKE. SIRI HII NI UKAMILIFU WA MWISHO WA VITU VYOTE HUKU MUNGU MWENYEZI AKIANGAMIZA WENYE DHAMBI WAASI NA KUANZISHA UFALME WAKE WA HAKI JUU YA ARDHI."




UFUNUO 10:8-11


NENDA UKALIPIME HEKALU LA MUNGU NA MADHABAHU, NA UHESABU WANAOSUJUDU HUMO. [1]
BALI USIONGEZE BEHEWA LILILO NJE WALA USILIPIME.
KWA MAANA IMEPEWA MATAIFA NA WATAUKANYAGA MJI MTAKATIFU KWA KIPINDI CHA MIEZI AROBAINI NA MIWILI. [2]
NAMI NITAWARUHUSU MASHAIDI WANGU WAWILI NAO WATATOA UNABII SIKU ELFU NA MIA MBILI NA SITINI HALI WAMEVIKWA MAGUNIA.
[1] HEKALU YERSUALEMU LITAKUWA LISHAJENGWA TENA NA HUKU KUPIMA KUNAASHIRIA UMILIKI WA MUNGU.
[2] MPINGA KRISTO NA JESHI LAKE WATACHUKUA YERUSALEMU NA HEKALU. WAYAHUDI WATAKAO ISHI WATAPEWA MAKAZI NA MUNGU HUKO NYIKANI. (UFUNUO 12:6, 14).


"NA YEYOTE ANAYEJARIBU KUWADHURU, MOTO HUTOKA KATIKA VINYWA VYAO NA KUWALA ADUI ZAO."
"MTU AKITAKA KUWADHURU HIVI NDIVYO IMPASAVYO KUUWAWA."


"HAWA WANA AMRI YA KUZIFUNGA MBINGU, KUYAGEUZA MAJI KUWA DAMU NA NA KUPIGA NCHI KWA KILA PIGO KATIKA SIKU ZA UNABII NA UCHUNGAJI WAO." [1]
[1] UANGALIFU KADHAA UNAPENDEKEZA KUWA MANABII HAWA WAWILI NI MUSA NA ELIYA.
1. WANAIPIGA NCHI NA PIGO KAMA MUSA, NA KAMA ELIYA WANAITA MOTO UJE CHINI KUTOKA MBINGUNI.
2. MUSA NA ELIYA WOTE WALIKUWA KATIKA KUGEUKA SURA KWA YESU.
3. WANAUME WOTE WAWILI WALITUMIA NJIA ZISIZO ZA KAWAIDA KUCHOCHEA TOBA.
4. KATIKA TAMADUNI YA KIYAHUDI WANAUME WOTE WAWILI WANGERUDI WAKATI UJAO.
5. UREFU WA UKAME ULIKUWA MIAKA MITATU UNUSU, SAWA NA ELIYA ALIVYOLETA ISRAELI.
6. ELIYA ALICHUKULIWA JUU MBINGUNI NA MUNGU ALIUZIKA MWILI WA MUSA AMBAKO HAUNGEPATIKANA.

"THE BIBLE EXPLAINED IN EVERY LANGUAGE."





SUPERBIBLE.TV